**5.0 MADHARA YA MAKOSA YA KIMTANDAO.**

• Huathiri maendeleo katika biashara mtandao, huduma za kibenki au mifumo ya malipo inapoingiliwa na husababisha hasara ya fedha na wateja pia hupoteza imani juu ya udhabiti katika mifumo ya TEHAMA.

• Kuingiliwa kwa faragha ya mtu, kuenea kwa chuki, kushusha utu wa mtu kutokana na picha za utupu zinazokiuka maadili au kutweza utu wa watu wengine.

• Makosa ya kimtandao huleta madhara katika siasa, kupitia mifumo ya utawala kwa njia ya mtandao wahalifu huweza kupotosha taarifa za Serikali.

• Makosa ya kimtandao hutumika kufanya matishio ya ujasusi au kuingilia mifumo inayotumika katika uchaguzi kwa kutoa takwimu ambazo si sahii.

**6.0 HITIMISHO**

Uhalifu wa kutumia mtandao umeongezeka kwa kasi sana katika jamii yetu, ni wajibu wa kila mwananchi kutumia vyema mtandao kwa ajili ya kuleta maendeleo chanya kwenye nchi yetu na si vinginevyo.


**Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :**

**Katibu Mtendaji,**
**Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania ,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,**
**Barabara ya Mkalama**
**S.L. P 1718**
**DODOMA**
**TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.go.tz**
**Tovuti: www.rlct.go.tz**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

# UHALIFU WA KIMTANDAO



**1.0 UTANGULIZI**

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

**2.0 UHALIFU WA KIMTANDAO**

Kwa kutambua umuhimu wa sheria kuakisi maendeleo ya sayansi na teknolojia, mnamo mwaka 2006 Tume ilifanya utafiti na kutoa Taarifa ya Mapitio ya Mfumo wa Sheria Zinazosimamia Miamala ya Kielektroniki na Makosa ya Kimtandao. Mwaka 2015, Bunge lilitunga Sheria ya Makosa ya Kimtandao. .

**3,0 AINA YA MAKOSA YA KIMTANDAO**

Makosa ya Kimtandao ni pamoja na;

**a) Uvamizi wa Kimtandao (Cyber trespass)**; kosa hili hufanyika kwa mtu asiyeruhusiwa kuwa katika mfumo wa mtandao fulani, anapoingia kwa kuiba neno siri na kuweza kupata nafasi ya kutumia mfumo ambao hana mamlaka ya kuingia.

**b) Uharamia wa Kimtandao (Cyber Piracy)**; kosa hili hufanyika kwa kuiba na kusambaza bidhaa zinazolindwa na sheria ya milki bunifu mfano, vitabu au nyimbo.

**c) Uharibifu wa Kimtandao (Cyber Vandalism)**; kosa hili hufanyika kwa kulenga kuharibu data na mifumo.

**d) Makosa ya Maudhui (Content)**; kosa hili ni la matumizi mabaya ya mtandao kwa kuweka maudhui yanayolenga , kupotosha, kufedhehesha au kushusha utu wa mtu kama vile:

- usambazaji wa picha za utupu;
- kashfa na taarifa za uongo; na
- makosa yenye kuashiria ubaguzi na kusababisha chuki katika jamii

**4.0 MAKOSA YA KIMTANDAO NA ADHABU ZAKE**

Sheria ya Makosa ya Kitandao imeainisha adhabu mbalimbali ambazo ni pamoja na;

• Matumizi ya mfumo wa kompyuta kinyume na sheria na adhabu yake ni faini ya shilingi milioni moja au zaidi au kutumikia kifungo gerezani kisichopungua miezi sita, au vyote kwa pamoja.

• Kuchapisha au kutoa ponografia za watoto na adhabu yake ni faini ya shilingi milioni hamsini au zaidi au kutumikia kifungo kisichopungua miaka saba au vyote kwa pamoja. Mahakama pia inaweza kutoa amri ya kumlipa fidia muathiriwa wa kosa husika.

• Kuchapisha au kusababisha kuchapishwa kwa ponografia na adhabu yake ni faini ya shilingi milioni ishirini au zaidi au kifungo kisichopungua miaka saba jela au vyote kwa pamoja.

• Kuchapisha taarifa za uongo kwa lengo la kupotosha, kusababisha chuki, kudhalilisha au kutisha na adhabu yake ni faini ya shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Mkurugenzi wa Mashtaka anamamlaka ya kufifilisha makosa muda wowote kabla ya mwenendo wa mahakama kuanza au kwa tamko la hiari la kukiri na kuamuru mtu huyo alipe kiasi cha fedha ambacho hakitazidi kiasi cha faini ya kosa husika. Ufifilishaji wa makosa unatakiwa uwe kwenye maandishi ukiambatanishwa na tamko la hiyari la kukiri kosa na uamuzi wa ufifilishaji ni wa mwisho na hautakatiwa rufaa.